# JINSI YA KUWAFUNDISHA WATOTO BIBLIA VIZURI

**Lugha:** Kiswahili


**Kimeandikwa na:** Katherine O'Donnell

**Kimehaririwa na:** Flavian Mkupasi & Edwin Msiri

**Wachoraji:** Jessica Bennett, Rebecca Talley & Katherine O'Donnell

**Kimetengenezwa kwa msaada wa machapisho kutoka:** Bible Translation and Literacy of East Africa & Katherine O'Donnell

**Maandiko yamechukuliwa kutoka:** Kiswahili Contemporary Version (Neno:



# Utangulizi

Mimi, Katherine O'Donnell, ambaye ni mwandishi wa kitabu hiki, ninafanya kazi na Wycliffe Bible Translators pamoja na Huduma ya Kutafsiri Biblia Katika Lugha za Asili Katika Mkoa wa Mbeya na Iringa, nchini Tanzania. Kwa uzoefu wangu katika Afrika ya Mashariki, nikiwa mwalimu wa walimu wa Shule za Jumapili, na mimi mwenyewe nikiwa mwalimu wa shule hizo; nilipoona umuhimu wa kuwa na vitabu vizuri vya Kiswahili kwa ajili ya kuwasaidia walimu, niliamua kuandika kitabu hiki.

Kwa sasa, kuna vitabu vya mitaala ya elimu ya Shule ya Jumapili kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo kitabu hiki si mtaala kwa ajili ya mafundisho ya Shule ya Jumapili, bali kimebuniwa na kuandikwa ili kitoe msingi wa namna ya kuwafundisha watoto kwa kutumia vitabu vichache vya kufundishia vilivyopo. Kitabu hiki kinaweza kutumika pamoja na vitabu vingine vya Shule ya Jumapili, na kuwapa walimu mbinu zaidi wanapoandaa masomo na kufundisha kufuatana na mitaala waliyo nayo. Pia kinaweza kutumiwa chenyewe kama kilivyo, kwani pamoja na mambo mengine, kitabu hiki, kinatoa pia mwongozo wa namna unavyoweza kutengeneza andalio binafsi la somo.

Kutokana na vipengele mbalimbali vilivyomo katika kitabu hiki, na ili kitabu hiki kiweze kutumika vizuri, ni vyema na lazima kitabu hiki kikatumika sambamba na kozi ya mafunzo ya walimu ili kuwapa walimu nafasi ya kuyafanyia mazoezi yale wanayojifunza. Hii itawafanya wawe na msimamo thabiti wakati watakapokuwa wakifundisha katika madarasa yao.

Ni matumaini yangu kwamba kitabu hiki kitawasaidia walimu kuufikisha ujumbe wa Neno la Mungu kwa watoto katika namna nyepesi na ya kupendeza.

Ni ombi langu kuwa, kwa neema ya Mungu, wale watakaotumia kitabu hiki watakuwa walimu waaminifu na wazuri wa watoto wanaopendwa na Mungu; na watafurahia kuona watoto wao wakikua katika imani na ufahamu kuhusu Mungu.

# Vitabu vingine vya Shule ya Jumapili

Vifuatavyo ni baadhi ya vitabu kadhaa vilivyo bora kwa ajili ya mtaala wa Shule za Jumapili, vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili:

***Tufundishe Watoto*** *(Central Tanganyika Press, Dodoma, Tanzania)*
Kuna mfululizo wa vitabu hivyo. Kila kitabu kina masomo hamsini na mbili (yaani, somo moja kwa kila wiki ya mwaka).

***Masomo ya Shule ya Jumapili kwa ajili ya Watoto*** *(Christian Learning Materials Centre, Kenya)*
Kuna mifululizo tofauti ya vitabu hivyo vinavyofaa kufuatana na umri tofauti wa watoto. Vitabu vya picha vinapatikana pamoja navyo.

***Kueni Katika Imani*** *(Central Tanganyika Press, Dodoma, Tanzania)*
Kuna mfululizo wa vitabu hivyo. Vitabu hivyo ni vya kufundishia Elimu ya Kikristo shuleni, lakini vinafaa kwa Shule ya Jumapili kwa ajili ya watoto pia.

Pamoja na vitabu hivyo kuna vitabu vingine vya Kiswahili vinavyofaa kwa watoto, kama vile vitabu vya sehemu za Biblia kwa watoto na hata vitabu vya picha na michezo. Pia kuna vitabu vya sehemu za Biblia katika lugha mbalimbali za asili, ambavyo vinavyopatikana kwa kuwasiliana na:

*Huduma ya Kutafsiri Biblia na Kuendeleza Lugha za Asili katika Mkoa wa Mbeya na Iringa, S.L.P. 6359, Mbeya, Tanzania*

# Yaliyomo


1. Umuhimu wa kuwafundisha watoto Neno la Mungu ………………..................... 1
2. Sifa za mtenda kazi wa watoto ........................................................................ 1
3. Namna watoto wanavyojifunza …………………………………………………… 1
4. Nidhamu ………………………………………………………………………….... 2
5. Sehemu tofauti za darasa moja la Shule ya Jumapili kwa ajili ya watoto…….... 2
6. Jinsi ya kupanga somo la Shule ya Jumapili.................................................... 3

   *Jambo la msingi (dhamira) katika mafundisho* ................................................ 4

   *Mafundisho* ........................................................................................................ 5

   *Kusimulia simulizi ya Biblia* ............................................................................... 7

   *Michezo* .............................................................................................................. 8

   *Kuomba* ............................................................................................................... 9

   *Mstari wa kukumbuka* ......................................................................................... 9

   *Kuimba nyimbo* ................................................................................................... 10

   *Kurudia walichojifunza wiki iliyopita* .................................................................. 11

   *Ratiba ya darasa la Shule ya Jumapili kwa ajili ya watoto* …………………..... 13

   *Mfano (A) wa ratiba* ........................................................................................ 14

   *Mfano (B) wa ratiba* ........................................................................................ 16

7. Kuwafundisha watoto kuhusu wokovu ............................................................. 17
8. Kueneza mafundisho ......................................................................................... 19

   *Kusaidiana kuboresha katika kufundisha kwenu watoto* ……………………….. 19

   *Kuwafundisha walimu wengine* …………………………………………………… 20

## 1. Umuhimu wa kuwafundisha watoto Neno la Mungu

Watoto wa leo ndio kanisa la kesho. Wanahitaji kupewa msingi imara ili wajenge imani juu yake. Ni upendeleo mkubwa kufanya kazi ya kuwasaidia watoto wamjue Mungu na kukua katika imani.

Kuna mistari mingi katika Biblia inayotukumbusha umuhimu wa kuwafundisha watoto Neno la Mungu:

- Mathayo 18:10-14
- Marko 10:14
- Methali 22:6
- Kumbukumbu la Torati 6:4-9; 31:12
- 2 Timotheo 3:14-15
- Zaburi 78:1-4

## 2. Sifa za mtenda kazi wa watoto

Kuwafundisha watoto Biblia ni jukumu kubwa na muhimu kama ilivyo muhimu kuwafundisha Biblia watu wazima.

**Mwalimu:**
- Ampende Yesu!
- Awe mwenye hekima na uvumilivu
- Awe mfano mzuri mbele ya watoto
- Awe mwenye wito wa utume
- Awe anasoma na anayelijua Neno la Mungu
- Awe anawaombea watoto mara kwa mara
- Awe mwaminifu katika kazi yake
- Akubalike na kuheshimiwa na jamii na wazazi wa watoto

**Ili kupata matokeo mazuri, mwalimu:**
- Awapende watoto na kuwa na uhusiano mzuri nao
- Awe mbunifu na mwenye kuwashirikisha watoto
- Awasaidie wazazi katika jukumu lao la kuwafundisha watoto wao
- Azungumze na wazee wa jamii na viongozi wa kanisa kuhusu darasa lao
- Apokee msaada na ushauri kutoka kwa viongozi wenye uzoefu na hekima

Akutane na walimu wengine ili kujadiliana matatizo, kubadilishana mawazo na kuomba kwa pamoja.

## 3. Namna watoto wanavyojifunza

Watoto ni tofauti kuliko watu wazima, hawawezi kutulia na kusikiliza kwa muda mrefu. Hivyo, ili kuvuta usikivu wao ni lazima mwalimu atumie mbinu mbalimbali za kuwafundisha, hii ni pamoja na kufanya masomo yawe mafupi. Ni lazima mwalimu azingatie kuwa anawafundisha watoto na hawahubiri watoto. Watoto hujifunza.....
- *Kidogo cha kile wanachosikia*
- *Nusu ya wanachosikia na kuangalia*
- *Zaidi wakisikia, kuangalia na kufanya*
- *Sana wakisikia, wakiangalia, wakifanya na kusema au kuzungumza.*

Kwa hiyo, unapoandaa somo na kufundisha, ukumbuke kuwashirikisha kwa…
- *Kutumia vitu wanavyoweza kuona na kugusa*
- *Kuwasaidia watoto kuongea na kujadili kuhusu wanachojifunza*
- *Kufanya shughuli zinazohitaji kutumia mikono*

Vitu hivyo vitawasaidia watoto kujifunza na kukumbuka vizuri zaidi. Pia ni muhimu uandae masomo vizuri ili yawe yawafae na kuwafurahisha watoto. Wakati unapoandaa, ni muhimu kuzingatia umri wa watoto. Watoto wa umri mkubwa wanaweza kukaa na kusikiliza kwa kipindi kirefu kiasi kuliko watoto wa umri mdogo. Usimulie simulizi kwa kiasi cha muda kulingana na umri wa watoto. Yaani, watoto wenye miaka mitano, wanaweza kukaa na kusikiliza kwa dakika tano, pia unahitaji kufanya kitu cha kuwashirikisha watoto, ili usipotee usikivu wao. Vivyo hivyo, kwa watoto wenye miaka kumi, simulizi isizidi dakika kumi. Jambo la muhimu ni kuwa, mwalimu anapaswa kutumia lugha rahisi inayofaa kwa watoto (k.m. sentensi fupi, maneno mafupi) kufuatana na umri wao. Kama inawezekana, atumie lugha wanayotumia nyumbani, lugha mama (kilugha) au ile wanayoielewa kirahisi.

## 4. Nidhamu

Hakuna mtoto aliye mkamilifu! Katika kila darasa lazima kuna watoto wasumbufu na wenye tabia ambazo si nzuri sana. Ili kuhakikisha kwamba hawalisumbui darasa lote na kusababisha watoto wengine wasifurahi na kujifunza vizuri, tabia zisizo nzuri lazima zishughulikiwe. Hata hivyo, kwanza ni vema kujaribu kuhimiza tabia nzuri kwa kutumia vivutio mbalimbali vitakavyowafanya wabadilike, kwa mfano, ‘chati ya tuzo’. Mapendekezo mbalimbali kwa ajili ya kuhimiza tabia njema na kukemea tabia mbaya yanafuata hapa chini.

Yafuatayo ni mawazo tu, labda hayatafaa kwa kila utamaduni au mazingira, na mbinu tofauti zinafaa kwa watoto tofauti. Kwa hiyo kwa umakini mkubwa chunguza na uone ni mazingira yapi na ni mbinu gani ingefaa kutumika kwa ajili ya watoto wako.

**Namna ya kuwatia moyo watoto ili wawe na tabia nzuri**

Tumia ‘jedwali la tuzo’: Watoto wanapata alama (kwa mfano, nyota) kwa kuhudhuria, kuwa na tabia nzuri, kuwa wapole, kuwasaidia watu, kujibu maswali n.k. Baada ya miezi kadhaa utoe tuzo kwa mtoto aliyepata alama nyingi zaidi kuliko wengine wote au mtoto anapopata alama kadhaa (kama 20) anapokea cheti cha mafanikio au tuzo ndogo. Pia, unaweza kutumia jedwali hilo kuvunja moyo tabia mbaya walizonazo watoto, kwa kuwaambia, kwa mfano, “Ukiendelea kufanya hivi, hutapata alama nyingi.”

**Namna ya kuadhibu tabia mbaya**

- Maelekezo ya sura, sauti ya ukali n.k.
- Kama kuna kiongozi mwingine, akae na mtoto asiyetulia (hasa wakati wa vipindi vizito)
- Mhamishie mtoto mbele, ili uweze kumwona kwa urahisi
- Kama wanaendelea kutotulia na kutosikiliza, uzungumze nao, uwaulize, “Kwa nini unatenda/unafanya/uko hivi?” Uzingatie mazingira ya nyumbani kwao. Je, wanataka kuja? Wanaweza kuchagua kuja au kutokuja. Mweleze mtoto jinsi anavyowasumbua wenzake kutokana na tabia yake.
- Ikiwa mtoto ataendelea kuwa na tabia mbaya, unaweza kumwagiza asihudhurie mafunzo wiki inayofuata

**Namna ya kuwafanya watoto wakae kimya:**

- Chagua ishara kuashiria kuwa unataka watoto wawe ukimya (kama vile kuweka kidole mdomoni). Ukiwataka watoto wakae kimya, upige makofi, halafu uweke kidole chako mdomoni na kusubiri mpaka watoto wote wamekuona na kuweka vidole vyao mdomoni pia.

## 5. Sehemu mbalimbali za darasa moja la Shule ya Jumapili kwa ajili ya watoto

Somo la Shule ya Jumapili linaweza kuwa na sehemu nyingi. Ni vizuri kutumia shughuli mbalimbali na mbinu tofauti katika kuwafundisha watoto. Somo linaweza kuwa na:

- Marudio ya walichojifunza wiki iliyopita (kwa kifupi)
- Maombi
- Simulizi
- Mafundisho
- Michezo (hasa michezo inayohusiana na mada unayowafundisha)
- Nyimbo (zinazohusiana na ulichofundisha)
- Mstari wa kukariri
- Shughuli itakayowasaidia watoto kukumbuka walichojifunza (k.m. Igizo, Sanaa, Chemsha bongo)

## 6. Jinsi ya kupanga somo la Shule ya Jumapili

Ni lazima uandae vizuri. Ili ufundishe vizuri unapaswa kuandaa somo siku kadhaa kabla ya darasa ili kuhakikisha kuwa umejipa muda wa kutosha kutafakari somo utakalofundisha na kuandaa chochote kitakachohitajika.

Kuna vitabu vinavyopatikana kuwasaidia walimu kuandaa masomo mazuri (vitabu hivyo ni kama vile vilivyoorodheshwa mwanzoni mwa kitabu hiki). Lakini, ukihitaji kuandaa wewe mwenyewe, yafuatayo yatakusaidia. Unapaswa kuandaa ratiba ya kutumia unapofundisha, kwa kufuata hatua hizi zifuatazo. (Kuna mifano ya ratiba katika ukurasa 13-16).

1. Chagua mistari ya Biblia utakayofundisha.
   a. Ni vizuri kutumia mada moja kwa wiki kadhaa. Kufanya hivyo kutawasaida watoto kukumbuka wanachojifunza. Kwa mfano:
      i. Soma mifano ya Yesu Kristo (mfano mmoja kila wiki)
      ii. Soma kuhusu maisha ya nabii fulani (kila wiki soma sehemu moja ya maisha yake)
      iii. Wokovu (kwa miezi kadhaa fundisha mpango wa Mungu wa wokovu kwa ajili ya binadamu, kuanzia mwanzo mpaka mwisho, ukiangalia mambo ya msingi ya historia ya wokovu kama vile anguko la mwanadamu, watu waliochaguliwa na Mungu, Kutoka utumwani na mengineyo)
      iv. Soma barua ya Paulo, kifungu kimoja kila wiki (kwa watoto wakubwa)
2. Anza kuandaa ratiba yako kwa kuandika mistari ya Biblia utakayotumia.
3. Soma mistari ya Biblia hiyo, mwombe Mungu akusaidie kuelewa Neno lake na kuandaa vizuri, kisha soma mistari hiyo tena ili kushika vizuri maneno na maana yake.
4. Tafuta dhamira au jambo la msingi la masomo ya kufundisha (jambo linalofaa kwa umri wa watoto na kugusa maisha yao) kutoka katika mistari hiyo (soma kurasa 4-5).
5. Tafakari jinsi ya kufundisha dhamira hiyo (soma kurasa 5-6). Pia zingatia haya yafuatayo:
   a. Namna gani utaoanisha somo lako na maisha ya watoto?
   b. Utafundishaje? (Utatumia mbinu gani?)
6. Kisha, tafakari kuhusu sehemu zingine za somo utakazotumia (sehemu zilizoorodheshwa katika ukurasa 3) na umalize ratiba yako kwa kuandika kila utakachofanya na kufundisha. Uandike kwa undani, ili usisahau unachotaka kufanya na kusema unapofika darasani. Zingatia haya:
   a. Jinsi ya kusimulia simulizi ili utunze usikivu wa watoto (soma kurasa 7-8)
   b. Jaribu kuhakikisha kwamba kila sehemu ya darasa inafuata dhamira hiyo; shughuli zote zifuate dhamira ya somo kadiri inavyowezekana
   c. Tumia shughuli mbalimbali na kuwashirikisha watoto
   d. Kuwa mbunifu – tumia vitu vya kufundishia vinavyopatikana katika mazingira yako – nyumbani, kanisani, bustanini au shambani

e. Nyakati zote uzingatie umri wa watoto na uwezo wao wa kuelewa
f. Hakikisha shughuli unazochagua zinafuatana katika namna yenye mantiki. (Kwa mfano, ufundishaji ni lazima ufuate baada ya kusoma simulizi!)

7. Rudia ratiba uliyoandaa. Angalia kama kuna vifaa vya kuandaa au mazoezi ya kufanya kabla ya darasa.
8. Kabidhi maandalizi yako mikononi mwa Mungu na kuwaombea watoto ili waweze kuelewa somo na kulitekeleza katika maisha yao.

Ikiwa walimu tofauti wanafundisha kila wiki, unapaswa kujua kile ambacho kila mwalimu anafundisha ili usitofautiane na wengine katika kufundisha kwako. Itakuwa vizuri ikiwa mtapanga kwa pamoja kile mtakachofundisha wiki zijazo, ili ufundishaji wenu uendane miongoni mwenu kila mmoja.

## *Jambo la msingi (dhamira) katika mafundisho*

Ili watoto wajifunze na kuelewa vizuri, ni lazima tuwafundishe kwa njia rahisi. Tunahitaji kuzingatia: “Tunawataka watoto wakumbuke kitu gani kimoja, kutoka katika masomo hayo wanapoondoka baada ya darasa?”

Ukijaribu kufundisha mambo mengi, watoto watachanganyikiwa na baadaye hawatakumbuka kitu chochote. Ni bora kuchagua kitu kimoja na kusisitiza kitu hicho mara nyingi.

Kitu hicho (yaani dhamira ya somo au jambo la msingi) kiwe rahisi kwa watoto kuelewa ili uweze kuwaelezea vizuri na kuwafafanulia maana yake.

Uchague dhamira ya somo kwa uangalifu kwa kuzingatia mambo haya mawili:
1. Dhamira ihusiane na mistari uliyosoma
2. Dhamira iwe na uhusiano na maisha ya watoto

**1. Dhamira ihusiane na mistari ya Biblia uliyosoma – Neno la Mungu litumike kwa usahihi**
Tunaposoma Neno la Mungu ni muhimu tusisome mstari mmoja tu bali tuzingatie pia mazingira yake, utamaduni wa nyakati za kibiblia na kusudi la mwandishi. Tusipofanya hivi, ni rahisi kukosa maana ya mistari tuliyosoma na kuwapotosha watoto tunaowafundisha.

> ***Mfano:***
> Tukitaka kuwasomea watoto mfano wa Msamaria Mwema, jambo la msingi la kufundisha ni nini? Ukisoma haraka bila kuzingatia kusudi la Yesu aliposimulia hadithi hiyo, pengine unaweza kuitumia hadithi hiyo kufundisha kwamba, tujihadhari tunaposafiri! Lakini, ukiisoma kwa uangalifu, na ukatumia maneno ya Yesu kwa usahihi, utaweza kufundisha kuwa tuwapende jirani zetu – na hiyo ndio dhamira ya hadithi hiyo.

**2. Dhamira iwe na uhusiano na maisha ya watoto**
Mnapoandaa ni lazima mzingatie maisha ya watoto wenu, kwa sababu mnatakiwa kuwaonyesha watoto wenu jinsi dhamira ya somo inavyohusika katika maisha yao. Ikiwa hawatambui jinsi Neno la Mungu linavyoyahusu maisha yao, hawatapenda kulisoma!

Dhamira au jambo la msingi linaweza kuwa moja kati ya aina tatu. Ili uweze kukumbuka, kila moja huanza na ‘T’.

**Tenda** – Jambo la msingi (dhamira) linaweza kuwa kitu fulani ambacho watoto lazima wawe wanaweza kutenda. Kwa mfano, linaweza kuwa juu ya kusoma Biblia, kusali, kuwasaidia wengine, kusema ukweli n.k.

> ***Mfano:***

Hadithi ya Msamaria Mwema: Jambo la msingi ni kumpenda jirani yako. Kwa hiyo, unapowafundisha watoto kutokana na hadithi hii, uwasaidie watoto kufikiri jinsi wanavyoweza kuwa majirani wazuri katika mazingira yao. Kwa mfano, wanapokuwa shule, wanawezaje kuwa rafiki wazuri? Ikiwa kuna mtoto mmoja ambaye hapendwi na watoto wengine na ana tatizo na masomo yake, wafanye nini kumsaidia ili awe kama Msamaria Mwema? n.k.

**Tabia** – Jambo la msingi linaweza kuwa, kama vile, *tabia* ya Mungu. Kwa mfano, linaweza kuhusu jinsi Mungu alivyo mwenye neema, aliyejawa na mamlaka, Hakimu, Mfalme n.k. Jambo la msingi au dhamira inapohusu tabia ya Mungu, mara nyingi hupelekea sisi kumwabudu na pia hutusaidia kusali/kuomba.

***Mfano:***
Simulizi ya Shadraka, Meshaki na Abednego waliotupwa katika tanuri lililokuwa likiwaka moto: Jambo la msingi ni kwamba Mungu ni mwaminifu. Kwa hiyo, unapowafundisha watoto kutokana na habari hii, ni vyema ukawasaidia watoto kuelewa jinsi uaminifu ulivyo (kwa kutumia mifano kutoka katika maisha yao). Pia, uwaongoze katika kumwabudu Mungu kwa uaminifu wake na jinsi tunavyoweza kumkaribia Mungu muda wote kwa sababu hatatuacha kamwe.

**Taarifa** – Jambo la msingi linaweza kuwa taarifa kuhusu Mungu. Kwa mfano, linaweza kuwa Yesu yu hai, au kwamba Mungu aliumba kila kitu. Jambo la msingi linapokuwa taarifa kuhusu Mungu, huwasaidia watoto kuelewa zaidi kuhusu yeye, na mara nyingi hutuongoza ili tuweze kumsifu.

***Mfano:***
Simulizi ya uumbaji: Jambo la msingi ni kwamba Mungu aliviumba vyote. Hivyo unapowafundisha watoto kutokana na habari hii uwasaidie watoto kufikiria vyote alivyoviumba Mungu kwa kuangalia mazingira yao. Kisha uwaongoze katika kumsifu na kumshukuru Mungu kwa sababu ya aliumba vitu mbalimbali.

Vitu vyote vingine darasani vitokane na jambo hilo – yaani, shughuli unazochagua kutumia (michezo, sanaa, mstari wa kukumbuka, nyimbo n.k.) zihusiane na kusudi la somo. Kwa hiyo ni bora zaidi kuchagua jambo la msingi la somo kwanza, kwa sababu itakuwa rahisi zaidi kupanga shughuli zingine kufuatana na jambo hilo la msingi.

## *Mafundisho*

Ni muhimu sana kuwasaidia watoto kufikiri jinsi simulizi na dhamira yake inavyogusa maisha yao (kama inavyosema hapo juu – yaani, iwe na uhusiano au iendane na maisha ya watoto). Wafikiri jinsi wanavyoweza kutumia walichojifunza katika maisha yao ya kila siku – nyumbani, shuleni, katika familia zao, pamoja na jirani zao au rafiki zao. Unapoandaa masomo ujiulize maswali kama: Watoto wanafanya nini kila siku? Wana wasiwasi kuhusu nini? Wanakutana na watu gani? Wanateswa vipi? Wanakabiliwa na mambo gani? Wanahitaji kujifunza nini ili wasaidiwe katika maisha yao ya kila siku? Wanahitaji kujifunza nini kuhusu Mungu ili waweze kumjua vizuri na kukua katika imani yao?

Unapowafundisha watoto, ni lazima uwafundishe jambo la msingi au dhamira ya somo katika namna ambayo itawasaidia kuelewa, kuona uhusiano wa dhamira iliyoiandaa na maisha yao na ambayo watakumbuka. Kuna njia mbalimbali za kufanya hivyo. Kwa mfano:


- Linganisha maisha au vitendo vya watu katika simulizi na maisha ya watoto. Kwa mfano, ukifundisha simulizi ya mnara wa Babeli, uwaelezee watoto kuwa simulizi hii inaonyesha athari ya majivuno na kiburi na kudhani kuwa tunaweza kufanya vitu vikubwa wenyewe bila ya msaada wa Mungu.
- Waulize watoto maswali ya kuwasaidia kutafakari simulizi na jambo la msingi, maswali kama: Ungejisikiaje ikiwa kitu hiki kingetokea kwako? Ungefanya nini? Kwa mfano, ukifundisha hadithi


ya Msamaria Mwema, uwaulizie watoto maswali kama, “Tukiona mtu mwenye tatizo, ambaye hatumpendi (kwa mfano shuleni, darasani), tufanye nini?”

- Kielelezo unachoweza kukiona. Tumia vitu vya kawaida vinavyopatikana nyumbani, shambani na katika mazingira yako. Uwe mbunifu!

***Mifano:***


Andaa kopo kwa kubadilisha alama kwenye kopo, ili ionyeshe kitu tofauti kuliko yaliyomo ndani ya kopo. Unaweza kutumia kielelezo hiki kuonyesha jinsi watu wanavyoangalia uzuri wa nje, lakini Mungu hutazama moyo (I Samueli 16:7).





Kufundisha kwamba Yesu ndiye nuru ya ulimwengu, ulete taa kutoka nyumbani.

Kufundisha kwamba bila Mungu hatuna uwezo, ulete tochi yenye betri. Kabla ya kuanza, ondoa betri. Waulize watoto, “Kwa nini haifanyi kazi?” Kama betri zinavyotoa uwezo kwa ajili ya tochi, vivyo hivyo, Roho Mtakatifu ndani yetu anatuwezesha.



Kufundisha jinsi tunavyohitaji kulisha Neno la Mungu ili tukue kiroho, andaa mimea miwili. Mmoja wenye maji ili ukue, mmoja bila maji ili unyauke. Neno la Mungu ni kama maji/chakula.



- Shughuli (kama igizo)

***Mfano:***
Ukifundisha hadithi ya Msamaria Mwema, watoto wajichukulie kama vile wako shuleni, na mtoto mmoja awe mtoto asiyependwa na wengine. Watoto wengine waigize namna wanavyo weza kuwa Wasamaria wema katika mazingira haya kwa mtoto huyo.

- Michezo

***Mfano:***
Ikiwa jambo la msingi la kufundisha ni kuhusu imani, unaweza kutumia mchezo unaopima imani yao kwa wenzao. Mtoto mmoja afunge macho yake wakati mwenzake anamwongoza, kwa kushika mkono wake. Watembee na kuzunguka. Mtoto aliyefunga macho yake anapaswa kumwamini mwenzake asimsabibishe kugongana na mwingine au samani (fanicha)!
Kwa kutumia michezo hiyo watoto wanajifunza maana ya imani, na unaweza kuwafundisha kuhusu kumwamini Yesu Kristo awaongoze katika maisha yao.

Baada ya kuomba na kufikiria kwa makini kuhusu jambo la msingi na namna ya kufundisha jambo hili katika namna inayoendana na watoto, sehemu nyingine iliyobaki ya somo inaweza kupangwa. Katika kurasa zinazofuata ni mawazo ya kila sehemu ya somo la Shule ya Jumapili. Katika ukurasa wa 13 utakuta ratiba iliyo wazi ambayo unaweza kuitumia kukusaidia wakati unapondaa somo la Shule ya Jumapili. Pia, kuna mfano wa mpango kwa ajili ya somo zima la Shule ya Jumapili.

## *Kusimulia simulizi ya Biblia*


Tunaposimulia simulizi, tunataka watoto waielewe na kuikumbuka. Kama inafaa, utumie lugha ya asili au ile wanayoitumia wanapokuwa nyumbani ili watoto waelewe vizuri. Tunaweza kutumia mbinu mbalimbali za kuwavutia watoto, ili wasikilize na kuelewa vizuri. Zifuatazo ni mbinu za kutumia ili kusimulia simulizi, lakini pia mbinu kadhaa miongoni mwa hizi zinafaa katika mafundisho au marudio. Pia, unaweza kutumia mbinu moja pamoja na nyingine.

- Simulia kwa mtindo wa kitamthilia unaovutia
    - Jua na kuielewa simulizi vizuri
    - Ili kuwavutia watoto na kumaliza vizuri, chagua yako ya kwanza na ya mwisho kwa umakini. Hii ni kwa sababu watu hukumbuka wanachosikia mwanzoni na mwishoni.
    - Zungumza kwa nguvu tofauti za sauti (paaza sauti, punguza sauti, zungumza haraka haraka au taratibu)
    - Simulia kwa mwonekano tofauti tofauti wa sura
    - Simulia kuhusu rangi, harufu, ladha, vitendo vya watu vinavyotokea katika simulizi, ili watoto waweze kudhani kuwa wako katika mazingira ambako simulizi hiyo ilitokea.
    - Eleza jinsi ambavyo wahusika walijisikia ipi
    - Unaposimulia hakikisha unawatazama watoto usoni mwao moja kwa moja

- Tumia vitendo

    ***Mfano:*** Mwanzo 1: Kuumbwa kwa dunia. Tumia vitendo kuwakilisha kila siku ya uumbaji.

    ***Mfano:*** Mfunike macho mtoto mmoja awe katika taswira ya kipofu. Mwambie mtoto ajaribu kwenda upande wa mwalimu, bila kuangalia.




- Tumia vitambaa vya rangi mbali mbali

    ***Mfano:*** Marko 4:35-41: Yesu anaamuru dhoruba itulie. Tumia kitambaa cha rangi ya bluu kuwakilisha maji ya ziwa. Unaweza kukung'uta kitambaa kuonyesha jinsi mawimbi yanavyokuwa wakati wa dhoruba n.k.
- Tumia sauti mbali mbali

    ***Mfano:*** Yesu alipoingia Yerusalemu kwa shangwe. Tumia, vigonganishe ili viwe kama sauti ya makwato ya mwanapunda.

    ***Mfano:*** Yesu anaamuru dhoruba itulie. Tumia ngoma kutoa sauti ya dhoruba, au kupiga makofi au miguu.
- Maswali – tumia maswali kuwafanya watafakari na washiriki katika simulizi husika.
- Picha za simulizi – unaweza kupata picha kwa:
    - Kutumia vitabu
    - Kuchora wewe mwenyewe kwenye ubao wa kuandika au karatasi
    - Kuomba mtu kanisani anayeweza kuchora vizuri achore picha kwa ajili yako, ili uzitumie darasani.

    ***Mifano:***






- Vitu vinavyohusiana na simulizi

    ***Mfano:***

Chagua vitu vinavyoendana kwa pamoja (k.m. sahani, kikombe, kijiko). Weka kwenye mfuko. Waombe watoto wachukue vitu mfukoni, kimoja baada ya kingine. Halafu, watoto waeleze jinsi vinavyoendana kwa pamoja (k.m. chakula). Vitu hivyo vitambulishe simulizi (k.m. Karamu ya Bwana, Mfano wa karamu ya harusi) na kutumika wakati unaposimulia.

***Mifano mingine:***
Ifuatayo ni mifano ya vitu vya kutumia wakati unaposimulia simulizi:

  - Kuwalisha watu elfu tano: Tumia mkate na kikapu
  - Yesu anamponya mtu aliyepooza: Tumia mkeka

- Igizo – igiza simulizi wakati unapoisimulia
  - Mwenyewe
  - Kwa kutumia watoto – watoto wanaweza kufanya mazoezi ya kuigiza (kwa kutumia maneno yao) au mwalimu anaweza kusoma Biblia wakati watoto wanaigiza anachosoma yeye.
- Maneno – andika maneno makuu kwenye karatasi au ubao wa kuandika
- Simulizi zinazojulikana – kama watato wanafahamu simulizi utakayosimulia, labda unaweza:
  - Kuwafanya wakusimulie simulizi hiyo. Mtoto mmoja aanze, na baada ya sentensi chache, mtoto mwingine aendelee n.k. Mwishowe watoto kadhaa watakuwa wamesimulia, na hivyo kuhusika.
  - Kusimulia simulizi, lakini uingize makosa. Watoto wajaribu kuona makosa yako
  - Kuwaomba watoto waigize simulizi

## *Michezo*

Watoto wanapenda sana michezo! Kwa kutumia michezo, itasaidia kuwavuta watoto wafike darasani. Wakiwa hapo, watapata nafasi ya kulisikia Neno la Mungu! Michezo huburudisha sana, lakini ina umuhimu mwingine pia. Zifuatazo ni sababu zinazofanya tucheze michezo mbalimbali:

- Mchezo ni shughuli ya kufanya wakati unapowasubiria watoto wote wafike
- Michezo inatumika kuwaamsha watoto au kuwatuliza (inategemea aina ya mchezo)
- Michezo inatumia nguvu za watoto ili waweze kukaa na kutulia baadaye
- Michezo inawasaidia watoto kujifunza kuhusu jinsi ya kushirikiana, kusikilizana, kutumia ubunifu wao, kuaminiana, kushinda na kushindwa bila kujisifu au kukasirika
- Unaweza kuitumia kutangulia/kutambulisha simulizi ya Biblia

  ***Mfano:***
  Simulizi kuhusu Yesu alivyomponya mtu aliyepooza: Cheza mchezo unaotumia miili yao mizima (k.m. kufuata vitendo vya kiongozi). Halafu ueleze namna sisi tulivyoweza kufanya vitendo vingi na kutumia kila sehemu ya mwili, lakini katika simulizi watakayosoma leo, kuna mtu mmoja aliyeshindwa kufanya kitu chochote kwa sababu alipooza, lakini Yesu alimsaidia.
- Unaweza kutumia mchezo unaohusiana na jambo la msingi la kufundisha ili kuwasaidia watoto kuelewa jambo hilo na kulikumbuka (soma ukurasa wa 6 ili kupata mfano).

Mambo ya kuzingatia watoto wanapocheza:

- Nafasi ya kutosha
- Muda wa kutosha
- Vifaa (k.m. mpira)
- Lengo la mchezo
- Kuwatia moyo wote washiriki
- Umri wa watoto
- Idadi ya watoto

## *Kuomba*

Watoto wafundishwe kuwa kuomba ni kuongea na Mungu, lakini wamwombe kwa heshima. Unapoomba, utumie maneno rahisi na maombi mafupi ili watoto waweze kuelewa, hakuna haja ya kutumia sala ndefu zinazoweza kuwachanganya watoto! Kujifunza kuhusu jinsi ya kuandaa maombi au sala, soma mafundisho ya Yesu kuhusu maombi katika Matayo 6:5-15.

Unapowaomba watoto wasali, kumbuka kwamba watoto kadhaa wanapenda kuomba kwa sauti, watoto wengine wanapenda kuomba kimya kimya, yaani mioyoni mwao. Kwa hiyo usiwalazimishe watoto kuomba kwa sauti.

Uwahimize watoto wakuambie mahitaji ya maombi yao, ili mfanye maombi pamoja kwa ajili ya mambo haya, na ili wewe mwalimu ukawaombee ukiwa nyumbani. Uwahimize watoto kuomba watakapokuwa nyumbani pamoja na familia zao na kulisimulia darasa zima la Shule ya Jumapili kuhusu majibu mbalimbali waliyoyapata kutokana na maombi yao, ili ninyi nyote mpate moyo wa kuendelea kuomba. Pia, kabla ya kusoma Biblia pamoja, mmwombe Mungu awasaidie kuelewa Neno lake (Zaburi 119:18).


Aina za maombi:
- Maombi ya shukrani
- Maombi ya kuombea mahitaji na msaada
- Maombi ya kumsifu na kumwabudu Mungu
- Maombi ya kuwaombea watu wengine

Mungu anatujibu kwa njia tatu:
- “Ndiyo” – Atatupa tunachoomba kama ni mapenzi yake
- “Hapana” – Hatatupa kama siyo mapenzi yake, au kama ni kitu kibaya kwetu
- “Subiri” – Mungu anajua wakati sahihi wa kutupa tunachoomba

## *Mstari wa kukumbuka*


Kama inavyosema katika Zaburi 119:11, tuweke Neno la Mungu mioyoni mwetu. Ili kuwasaidia watoto kujifunza mstari vizuri, utumie mstari mmoja kwa wiki kadhaa – mstari unaofaa kwa dhamira/mada ya masomo. Pia, uzingatie umri wa watoto. Watoto wadogo wajifunze mistari mifupi, lakini watoto wakubwa wanaweza kujifunza mistari mirefu zaidi. Kuna mbinu nyingi za kujifunza mistari zinazofurahisha.

- Maneno yanayotoweka – Uandike mstari watakaojifunza katika ubao wa kuandika. Usome mara kadhaa pamoja na kuonyesha kila neno. Watoto wasome pamoja na wewe. Halafu ufute neno moja au mawili. Watoto wasome tena wakati unapowaonyesha kila neno, na unapofika maneno uliyofuta, waseme kwa kukumbuka tu. Uendelee kufuta kila neno mpaka mstari mzima umefutwa, na watoto waweze kusema bila kusoma.




- Vitendo – Tumia vitendo vinavyowakilisha maneno wakati unapokariri mstari. Watoto wavifanye, pamoja na mwalimu.
- Nyimbo – Tunga wimbo unaotumia maneno yale yale ya mstari mnaojifunza.
- Picha – Uandike mstari watakaojifunza katika ubao wa kuandika. Lakini,

badala ya kutumia maneno tu, uchukue nafasi yao na picha.





**Kurudia mistari waliyojifunza**

Ili kuwasaidia watoto kushika Neno la Mungu mioyoni mwao, ingesaidia ukitumia mstari mmoja kwa wiki kadhaa (badala ya kujifunza mstari mpya kila wiki). Unaweza kutumia mbinu zifuatazo kurudia mistari mliyojifunza.

- Waombe watoto wakuambie mstari waliojifunza. Labda mkariri pamoja kwanza, kwa kutumia mbinu zinazoandikwa hapo juu.
- Mchezo: Andika mstari kwenye karatasi. Gawa mstari kwa kukata karatasi (kama mfano ufuatao). Changanya maneno. Watoto wajaribu kupanga maneno kwa usahihi. Unaweza kufanya hivyo kama shindano. Watoto wagawanyike katika vikundi, kila kikundi kipewe mstari ulioandaa. Halafu ni kama mbio – kundi/timu gani watamaliza kuweka mstari sahihi kwanza?!

***Mfano:***




## *Kuimba nyimbo*

Kwa nini tuimbe?


- Watoto wanapenda kuimba
- Wote wanaweza kushiriki
- Kama watoto wanaanza kutotulia, kuimba wimbo huwasaidia kusikiliza na kutulia tena
- Mnapoimba nyimbo za kibiblia, watoto wanajifunza kweli za Biblia
- Unaweza kutumia nyimbo zinazohusiana na dhamira ya masomo, ili kuimarisha walichojifunza
- Kukumbuka *Mstari wa Kukumbuka* – ukitumia/ukitunga wimbo unaotumia maneno ya mstari ule moja kwa moja

Ni afadhali kuimba wimbo katika lugha wanayoifahamu watoto, lugha ya nyumbani / lugha ya asili, ikiwa hawaelewi Kiswahili vizuri. Kwa hiyo, kama hamna wimbo ulio katika lugha yao ya asili, ni vizuri kutafuta watu wanaoweza kutunga wimbo katika lugha yao. Ikiwa ni lazima kutumia Kiswahili, uwaelezee watoto maana ya nyimbo.


Mbinu za kuimba:

- Wote wanaimba pamoja au wagawanyike katika vikundi (k.m. wasichana na wavulana huimba sehemu tofauti za wimbo)
- Imba kwa vitendo vinavyoendana na wimbo
- Imba kwa maombi
- Piga makofi au tumia ala/vyombo vya muziki. Unaweza kutengeneza ala za muziki kwa kutumia vitu mbali mbali vinavyopatikana

***Mifano:***




Vifimbo vya kupigana | Vibuyu vya kutikisa | Kopo zinazojazwa mbegu, visoda, mawe madogo n.k. | Ngoma ndogo



Vifuu vya kugongana au piga na fimbo | Ala za muziki za kutikisa

## *Kurudia walichojifunza wiki iliyopita na walichojifunza katika darasa lile*

Ukirudia masomo ya wiki iliyopita utajua ikiwa watoto wanakumbuka walichojifunza na kurudia kunawasaidia watoto kujifunza vizuri zaidi. Pengine, kurudia masomo yaliyopita kutawaandaa watoto kwa ajili ya masomo ya leo (hasa kama unafuata kitabu au dhamira fulani).

Mbinu za kurudia:


- Uliza maswali (kuhusu masomo ya wiki iliyopita).
- Uliza maswali (kuhusu masomo ya wiki zilizopita) kwa njia ya shindano au chemsha bongo.

***Mfano:***
Weka visoda mfukoni (k.m. CocaCola x 5, Pepsi x 3, Fanta x 1). Watoto wagawanyike katika vikundi/timu mbili au zaidi. Kwanza, uwaulize timu A swali moja. Kama wanajibu kwa usahihi, mtoto aliyejibu aje mbele na kutoa kisoda kimoja kutoka katika mfuko (bila kuangalia). Akipata kisoda cha CocaCola, timu yake hupata pointi 1, akipata kisoda cha Pepsi, timu yake hupata pointi 5, akipata kisoda cha Fanta, timu yake hupata pointi 10. (Baada ya kukitoa kisoda, akirudishie kwenye mfuko). Halafu, unandelea na timu B n.k. Mwishoni, uhesabu pointi za kila timu ili kujua ni timu ipi imeshinda.


***Mfano:***
Andaa kauli/maelezo ambayo ni 'kweli' au 'uongo'. Watoto wasimame katikati ya chumba. Upande mmoja wa chumba upo 'kweli', na mwingine upo 'uongo'. Soma kauli/maelezo moja. Kila mtoto afikiri mwenyewe kama ni 'kweli' au 'si kweli', na akimbilie anaodhani ni sahihi kutokana na alivyoelewa maelezo.

***Mfano:***
Andaa maswali pamoja na majibu matatu au manne – majibu mawili au matatu yawe 'si kweli', jibu moja liwe sahihi. Kila pembe ya chumba ipewe jina, kwa mfano A, B, C na D, au 1,2,3 na 4. Soma swali moja pamoja na majibu. Kila mtoto afikiri mwenyewe kama jibu la A, B, C au D ni kweli. Kisha akimbilie kwenye pembe inayofaa.
*K.m. Yesu alizaliwa wapi? A)Yerusalemu B) Nazareti C) Bethlehemu D) Dar es Salaam*

- Onyesha picha za simulizi, waambie watoto wajadiliane au watoe maoni yao kuhusu picha hizo.
- Onyesha vitu vinavyohusiana na simulizi, kisha uliza, "Kitu hiki kinawakumbusha nini kutoka katika simulizi iliyopita ya Biblia?" Kwa mfano, fimbo ya mchungaji na lubega – vitu hivyo vingefaa kurudia mfano wa kondoo aliyepotea.
- Igiza simulizi ya wiki iliyopita.
- Andika maneno muhimu ya simulizi kadhaa. Kisha watoto wajaribu kutafuta maneno yanayolingana kutoka hadithi moja.




- Sanaa: Watoto wanapenda sana kufanya sanaa na sanaa zinawasaidia watoto kukumbuka walichojifunza. Ukifanya sanaa uzing
- Vifaa vinavyopatikana kwa urahisi
  - o Utunze vitu vyote nyumbani – usitupe chupa, boxi au magazeti! Unaweza kutumia vitu vingi kwa ajili ya sanaa!
  - o Unaweza kutumia vifaa vya viumbe vyote, k.m. mawe, gamba la konokono, majani, maharage n.k.






- Watoto wangapi? – Kuna nafasi za kutosha kufanya sanaa na wasaidizi wa kutosha (hasa kwa watoto wadogo)? n.k.
- Usalama na usafi
- Jinsi sanaa zinavyoweza kuhusiana na masomo

***Mfano:***
Tafuta picha za nyuso za watu (tumia magazeti), watu kutoka nchi mbali mbali. Watoto waambatishe kwenye karatasi. Halafu uweke ukutani. Tumia kukumbuka jinsi Mungu anavyopenda ulimwengu (Yohane 3:16), au jinsi Yesu alivyotuamuru kuwafanya watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wake (Mathayo 28:18-20).

***Mfano:***
Ukifundisha kuhusu jinsi Mungu alivyoumba dunia, chukua upande mkubwa wa karatasi. Watoto wakusanye vitu vingi kama majani, maharage, manyoya n.k. Andika katikati ya karatasi mstari Mwanzo 1:1 (tumia herufi kubwa). Watoto wapake rangi herufi, kisha wapambe karatasi kwa vitu walivyokusanya, na uchoraji.



## ***Ratiba ya darasa la Shule ya Jumapili kwa ajili ya watoto***

*Ufuatao ni mfano wa ratiba utakayoijaza wakati wa kuandaa somo la Shule ya Jumapili.*

Mada ya mfululizo wa masomo:

Aya ya Biblia:

Umri wa watoto:

Jambo la msingi/dhamira la masomo ya kufundisha:

**Mchezo**

**Rudia walichojifunza wiki iliyopita**
*(Njia za kufundishia/vitu vya kufundishia)*

**Maombi:** *Mungu afungue macho yetu ili tuelewe Neno lako*

**Simulia**
*(Njia za kufundishia/vitu vya kufundishia)*

**Mafundisho**
*(Njia za kufundishia/vitu vya kufundishia)*

**Nyimbo**

**Mstari wa kukariri**
*(Njia za kufundishia/vitu vya kufundishia)*

**Shughuli itakayowasaidia watoto kukumbuka walichojifunza**
*(Njia za kufundishia/vitu vya kufundishia)*

**Maombi**

**Michezo**

---

**Maandalizi**
*(Vitu vya kuandaa, mazoezi ya kufanya)*

## Mfano (A) wa ratiba

*Hapo chini ni mfano wa ratiba ya somo la Shule ya Jumapili kuhusu jinsi Mungu anavyotupenda sisi sote bila upendeleo. Mfano huu unakuonyesha jinsi kila sehemu ya ratiba inavyotakiwa kujazwa kwa umakini mkubwa ili ujiandae vizuri kwa kufundisha. Mfano mwingine unapatikana katika ukurasa wa 16.*

### 25 Januari 2009

Mada ya mfululizo wa masomo: Jinsi Mungu anavyotupenda

Aya ya Biblia: Yohana 4:3-15

Umri wa watoto: Miaka 7-11

Jambo la msingi la masomo ya kufundisha: Mungu anawapenda watu wote kwa usawa, hakuna tofauti kati ya watu, sote tumekuwa wamoja katika Kristo Yesu.

<u>Nyimbo</u>: Nyimbo zinazohusiana na mambo ya somo hili.

<u>Mchezo</u>: Kugawanyika katika vikundi vya kitu fulani.

<u>Utangulizi wa simulizi</u>

Rejea mchezo mliokuwa mmegawanyika katika vikundi vidogo, kila kikundi kilikuwa tofauti na kikundi kingine. Sisi sote ni tofauti. Tunaonekana tofauti, tuna umri tofauti, tunatoka mahali tofauti, tumepata elimu tofauti n.k. Lakini, tuna kitu kimoja ambacho ni kwa ajili ya wote. Mungu anatupenda.

<u>Maombi</u>: Mungu afungue macho yetu ili tuelewe Neno lake

<u>Simulia:</u>

Simulia moja kwa moja kutoka katika Biblia. Chagua watoto wawili kusoma maneno ya Yesu Kristo na Msamaria. Wawe na Biblia.

(Nyenzo: Biblia)

<u>Mafundisho:</u>

Uliza maswali:

- Yesu alikutana na nani kisimani?
- Alimwomba nini Msamaria?
- Mbona Msamaria alifikiri ombi la Yesu lilikuwa la ajabu?

Eleza kuhusu Wayahudi na Wasamaria, jinsi ambavyo hawakupendana. Sisi sote ni tofauti. Pengine hutuwapendi wengine kwa sababu hao ni tofauti - jinsi wanavyoonekana, wanavyosema, wanapotoka n.k. Lakini, tuangalie jinsi Yesu alivyojibu.

Uliza maswali:

- Je, Yesu alimdharau / alimfanyia mzaha / alimwacha?
- Kwa nini Yesu alimwonyesha wema yule Msamaria ingawa Wayahudi wengine wasingefanya hivyo?

Yesu hakujali kuhusu tofauti kwa sababu Mungu anatupenda sisi sote kwa usawa. Tukimwamini Yesu, sisi sote tumekuwa wamoja katika Kristo Yesu.

Mungu anatutaka kuwapenda wengine hata kama hao ni tofauti.

Maisha yako:

Kwa hiyo, shuleni, kama kuna watoto ambao ni tofauti na hawapendwi na wengine, mfanyeje?

Mstari wa kukumbuka: Wagalatia 3:28 – tumia vitendo

Shuguli itakayowasaidia watoto kukumbuka walichojifunza:

Andika mstari wa kukariri halafu weka ukutani. Watoto wachore watu wa aina tofauti kwenye karatasi. Weka picha zote za watoto kuzunguka mstari wa kukumbuka.

(Nyenzo: Karatasi na mstari wa kukariri, picha ya watu kwenye karatasi, chaki/penseli laini ya rangi/kalamu ya risasi na gundi ya karatasi).

Maombi

Mwishoni: Kariri ule mstari tena

Maandalizi

- Picha ya watu kwenye karatasi
- Andika mstari wa kukumbuka kwenye karatasi kubwa
- Pata chaki/penseli laini ya rangi/kalamu ya risasi na gundi ya karatasi
- Fanya mazoezi ya vitendo vya mstari wa kukumbuka
- Fanya mazoezi ya kusimulia simulizi

## Mfano (B) wa ratiba

# 31 Januari 2010

Aya ya Biblia: Luka 17:11-19

Umri wa watoto: 7-11

Jambo la msingi la masomo ya kufundisha: Kutoa shukrani kwa Mungu

Rudia walichojifunza wiki iliyopita: Fanya chemsha bongo, uliza watoto maswali kuhusu somo la wiki iliyopita. Wanapata pointi kwa kutumia visoda vya rangi tofauti.

Maombi: Mungu afungue macho yetu ili tuelewe Neno lake.

Simulia: Eleza 'ukoma' ni nini. Simulia katika maneno yangu, kwa kutumia vitendo.

Mafundisho:

- Wapa watoto pipi. Angalia kama wanasema 'Asante'. Halafu, zungumza kuhusu majibu yao – kama walisema asante au siyo.
- Halafu, fundisha kuhusu simulizi – mtu mmoja tu aliyerudi kusema asante.
- Tutoe shukrani tunapopokea kitu – kama ni kitu kikubwa kama uponyaji, au kitu kidogo kama pipi.
- *Tutoe kwa watu*. Toa mfano kuhusu wazazi (waulize watoto, wazazi wenu, wanapokupa chakula, usemaje?)
- *Tutoe kwa Mungu*. Watoto wataje vitu vya kumshukuru Mungu – k.m. chakula, familia.
- Uliza watoto: Tunazwezaje kumshukuru Mungu? (Jibu – kwa maombi, kutoa sadaka na nyimbo)

Maombi: Kila mtoto amshukuru Mungu kwa kitu kimoja katika maisha yake

Nyimbo: Asante Yesu

Mstari wa kukariri: Zaburi 118:29 (tunga wimbo na maneno hayo)

Mchezo: Kama muda ya kutosha – cheza 'Simoni anasema'

Maandalizi:


- Soma simulizi mara nyingi ili niweze kusimulia vizuri katika maneno yangu
- Tunga wimbo wa mstari wa kukumbuka
- Pata pipi


## 7. Kuwafundisha watoto kuhusu wokovu

Ni lazima tuwafundishe watoto kuhusu wokovu. Wanahitaji kujua wokovu ni nini na jinsi tunavyoweza kuokolewa. Wajifunze kuhusu neema na rehema ya Mungu na fadhili zake. Lakini, tuwaelezee watoto mambo hayo katika njia iitakayowafanya waelewe kwa urahisi. Maneno kama ‘neema’ na ‘fadhili’ ni maneno magumu kwa watoto kuelewa! Kuna njia mbalimbali za kueleza mambo haya na kuna simulizi nyingi za Biblia zinazofaa kutumika kuyaelezea mambo haya.

Hapo chini kuna mfano moja wa jinsi ya kufundisha kuhusu wokovu. Kuna hatua nne za kutumia. Unaweza kuzitumia kama mfululizo wa masomo kwa wiki nne. Kilichoandikwa ni muhtasari tu; ni lazima uongeze kufuatana na umri wa watoto. Kwa kila somo kuna mstari wa kukumbuka, lakini kwa watoto wadogo uchague mstari moja rahisi unaofaa kwa wiki zote nne. Pia, uweke alama ambayo ipo kwa kila wiki ili kuwasaidia watoto kukumbuka walichojifunza. Kila alama inawakilisha wazo kuu (au jambo la msingi) la somo moja. Kwa mfano, kwa somo la pili, □ inawakilisha makosa (kama alama atumiayo mwalimu kwa majibu yasiyo sahihi), ili iwasaidie watoto kukumbuka kwamba somo linahusu jinsi tulivyotenda dhambi (tulivyofanya makosa) na kwa hiyo tunamhitaji mwokozi. Kila wiki unaweza kuwaonyesha watoto alama kutoka katika wiki iliyotangulia na kuwauliza maswali ili iwasaidie kukumbuka kile walichojifunza.

Mwishoni kuna maswali ya kutumia kupima ufahamu wao kuhusu jambo hili na kuwapa nafasi ya kuitika. Lakini, tusiwalazimishe watoto waombe na kupokea wokovu. Watoto waamue wao wenyewe kama wako tayari kumpa Yesu maisha yao au la. Ni muhimu wakaelewa kwamba kuokolewa si kuomba maombi fulani tu, bali tunatakiwa kuomba na kutubu kwa dhati kutoka mioyoni mwetu. Ikiwa tunampenda Mungu mioyoni mwetu kwa dhati, maisha yetu yatabadilika na tutatamani kumtumikia Yeye.

| **Kuwafundisha kuhusu wokovu** | |
|---|---|
| **Alama** | **Maelezo** |
|  | Mungu ni nani?<br>• Mungu aliviumba vitu vyote<br>• Mungu ni mkamilifu, anayefanya mambo yote vizuri<br>• Biblia ni Neno la Mungu<br>• Mungu anakupenda<br><br>Mstari wa kukumbuka: ***Yohana 3:16a*** *“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu”* |
| **X** | Kwa nini tunamhitaji mwokozi?<br>• Sisi sote tumefanya dhambi, ninyi na mimi pia<br>• Dhambi ni kutomtii Mungu. (Waulize watoto, “Niambie kitu kimoja ulichofanya ambacho Mungu hapendi, yaani,ambacho tunaweza kukiita ni dhambi?”<br>• Dhambi zinatutenganisha na Mungu na kutuzuia kufika mbinguni, mtenda dhambi ataadhibiwa<br>• Huwezi kuiondoa dhambi yako wewe mwenyewe<br>***Warumi 3:23*** *“Kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.”* |

<table>
<tr>
<td></td>
<td>Mungu amefanya nini ili kutuokoa?<br>● Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, hakumkosea Mungu hata mara moja!<br>● Kwa sababu Yesu ni mkamilifu, aliweza kuwa dhabihu/sadaka kwa ajili yetu<br>● Kwa hiyo, alifika duniani na kusulubiwa kwa ajili yako, ili dhambi zako zisamehewe na Mungu. Aliadhibiwa badala yako.<br>● Siku ya tatu baada ya kufa kwake Yesu Kristo, alifufuka<br>● Sasa Yesu yu hai, na yupo mbinguni<br>1 Wakorintho 15:3-4 “Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yasemavyo Maandiko…alizikwa na alifufuka siku ya tatu.” Au…<br>2 Wakorintho 5:21 “Kwa maana Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.”</td>
</tr>
<tr>
<td>?</td>
<td>Jibu lako ni lipi?<br>● Kila mtu hapa anahitaji kuchagua mwenyewe atakachofanya. Kuamini au kutoamini.<br>● Ukitaka kumfahamu Mungu, unatakiwa kumwomba Yesu awe Mwokozi na rafiki yako, umfuate, na kutenda mapenzi yake. Umjibu Mungu kwa:<br>    ● Kujua kwamba umemkosea.<br>    ● Kumwamini Yesu Kristo kwamba ni Mwana wa Mungu na alikufa na kufufuka kwa ajili yako ili kuziondoa dhambi zako.<br>    ● Kumwambia “Nimekukosea naomba unisemehe nataka kukufuata siku zote za maisha yangu. Naomba uwe mwokozi wangu na Bwana wangu.”<br>Warumi 10:13 “Kwa maana, “Kila mtu atakayeliitia Jina la Bwana, ataokoka.””</td>
</tr>
<tr>
<td colspan="2">Maswali ya kutumia ili kupima uwezo wa mtoto kuelewa wokovu<br>● Dhambi ni nini? (Tunapofanya / sema / fikiri vibaya)<br>● Watu wangapi duniani wamefanya dhambi? (Wote, pamoja na mimi pia)<br>● Adhabu ya dhambi ni nini? (Mauti ya milele, kutenganishwa na Mungu)<br>● Yesu Kristo ni nani? (Mwana wa Mungu)<br>● Kwa nini Yesu alisulubiwa? (Kwa ajili yetu, ili dhambi zetu ziondolewe)<br>● Kwa nini ni Yesu tu, aliyeweza kufa kwa ajili yetu? (Kwa sababu hakuwa na dhambi)<br>● Nini kilitokea siku ya tatu baada ya kufa kwake? (Alifufuka)<br><br>Mtoto akielewa yote…<br>…ajue inachosema Biblia: “Mwamini Bwana Yesu nawe utaokolewa.” Matendo 16:31<br><br>Na kwamba…<br>● Mungu anasema inatubidi kufanya nini? Kumwamini Yesu Kristo.<br>● Yeye Mungu atatufanyia nini? Atatuokoa.<br><br>Kisha mtoto awe na nafasi kumjibu/kumwitikia Mungu.</td>
</tr>
</table>

Njia nyingine ya kueleza kuhusu wokovu na huruma ya Mungu ni kutumia hadithi au mfano kutoka maisha yao.

> ***Mfano:***
> "Fikiria...umekuwa mtoto mbaya kwa kumfanyia mzaha kaka yako. Baba yako akasikia ulichofanya, kisha akakuita ili akuadhibu. Lakini, kaka yako anamkimbilia baba na kusema, "Usimchape. Unichape mimi badala yake. Ninampenda sana, sitaki umuadhibu. Nimemsamehe." Upendo wa kaka yule kwa dada yake unafanana na upendo wa Yesu kwetu. Yesu ailkuwa tayari kuadhibiwa badala yetu ili tusamehewe kisha tuwe na urafiki na Mungu."

Usiishie hapo, haitoshi tu kuwaelezea watoto kuhusu wokovu. Mtoto akimwamini Mungu, atahitaji msaada ili akue katika imani yake na kujua jinsi ya kumfuata Yesu Kristo siku zote za maisha yake. Unahitaji kumsaidia ili akue katika uwezo wake wa kuelewa jinsi Mungu anavyompenda sana, na kutaka uhusuiano mzuri pamoja naye. Mtoto afikirie kwamba ukiwa na rafiki mzuri, unafanya vitu vingi pamoja naye, unaongea naye, na mnasikilizana. Ni vivyo hivyo ukiwa na urafiki na Mungu pia. Pia, mtoto anahitaji msaada katika kusoma na kuelewa Biblia, na kujua jinsi ya kumtii Mungu na kuomba. Lazima uwe mfano mzuri mbele ya watoto katika mambo hayo yote.

## 8. Kueneza mafundisho

Ikiwa walimu watapokea mafundisho ya kitabu hiki, ni vizuri ikiwa watakuwa wanakutana pamoja mara kwa mara ili waweze kusaidiana. Pia, mwalimu atafute nafasi ya kuwafundisha wengine ili mafundisho hayo yawafikie watu wengi ili watoto wengi wafaidike.

## *Kusaidiana kuboresha katika kufundisha kwenu watoto*

Utakumbukaje na kutekeleza ulichojifunza?

**Binafsi**
Kila wiki usome sehemu ya kitabu hiki. Jikumbushe mambo hayo na fikiria jinsi ya kuyatekeleza au kuyaboresha katika darasa lako.

**Pamoja na wengine**
Mkikutana pamoja mnaweza kusaidiana katika kazi yenu ya kufundisha. Kwa hiyo, labda mnaweza kupanga mkutano ili kutoa nafasi ya kuulizana maswali yafuatayo:

- Umetekeleza mabadiliko gani katika darasa lako?
- Mabadiliko gani yamefanikiwa? Na yamefanikiwa kivipi?
- Mabadiliko gani hayajafanikiwa? Kwa nini?
- Tunawezaje kuboresha masomo tunayofundisha?
- Una mawazo mapya ya jinsi ya kufundisha, shughuli au michezo mipya ya kutumia?
- Je, kuna mambo gani mapya kwa ajili ya Shule ya Jumapili ambayo walimu tungependelea kufundishwa zaidi?

Pia, mnaweza kufanya kazi pamoja ili kuwafundisha walimu wengine. Mjadiliane yafuatayo:

- Je, umeanza kumfundisha mwalimu mwingine kanisani kwako? Na maendeleo/hali ikoje?
- Je, tuendeshe warsha? Kufanya hivi, tufanye nini? (Zingatia mambo kama: Wapi? Lini? Nani atakayealikwa? Nani atakayefundisha? Tunahitaji vifaa gani?)

Mchague mratibu wa kuitisha mikutano kama hiyo na ambaye atafanya mawasiliano yawe mazuri miongoni mwenu.

## *Kuwafundisha walimu wengine*

Ili watoto wote wapate mafundisho mazuri katika Shule ya Jumapili, ni jukumu lako kama mwalimu wa watoto kuwafundisha walimu wengine ili mafundisho yasambae ili watoto wengi wafaidike.

**Fundisha walimu wapya kanisani kwako**

Katika makanisa mengi, kuna walimu wachache, kwa hiyo kuna madarasa machache na watoto wengi wa umri mbalimbali katika darasa moja. Watoto wa umri tofauti wanahitaji kufundishwa tofauti, kwa hiyo, ukiwafundisha walimu wapya kanisani kwako, utaweza kugawa madarasa kufuatana na umri wa watoto (kwa mfano darasa moja kwa watoto wa miaki 3-5, mengine kwa miaka 6-8, 9-12 na 13-15). Kwanza, unahitajika kutafuta watu ambao wangependa kuwafundisha watoto. Wawe watu wanaompenda Mungu, Neno lake, watoto wake na kuwa na mzigo kwa ajili ya watoto ili watoto wakue katika imani. Kisha utatakiwa kuwafundisha jinsi ya kuwafundisha watoto kwa kufuata hatua zifuatazo. (Uanze na mtu mmoja au wawili).

1. Wahudhurie darasa la Shule ya Jumapili ili kuangalia jinsi unavyofundisha.
2. Wakae pamoja nawe wakati unapoandaa somo ili wajue jinsi unavyojiandaa na kutayarisha somo.
3. Wafike darasani tena kuangalia jinsi unavyofundisha somo hilo (labda wanaweza kuongoza maombi au nyimbo).
4. Wakae pamoja nawe tena wakati unapoandaa somo. Uwaruhusu kukusaidia kuandaa somo kwa kujadiliana na kubadilishana mawazo pamoja nao.
5. Anza kuwapa majukumu ya kuongoza sehemu fulani ya darasa. Kwa mfano, kwa wiki kadhaa wapewe jukumu la kufundisha mstari wa kukumbuka, wiki zingine wasimulie simulizi. Baada ya darasa, uzungumze nao kuhusu jinsi walivyofundisha – kuwatia moyo na kufikiria jinsi ya kuboresha. Mwendelee kwa namna hiyo kwa miezi kadhaa mpaka wakati ambao watakuwa wameweza kuongoza kila sehemu ya darasa. Sehemu ya mwisho kuongoza iwe *mafundisho* kwa sababu sehemu hii inahitaji zaidi ya uzoefu na ufahamu mzuri wa Biblia na maisha ya watoto. Mwanzoni, uwasaide wanapoandaa sehemu yao ya kufundisha, lakini baada ya kujaribu wao mara mbili au tatu, waendelee peke yao.
6. Waandae somo zima pamoja nawe (lakini, usiwasaidie sana), kisha wawafundishe watoto ukiwa umekaa na kuaangalia tu wanapofundisha. Baada ya darasa mzungumze pamoja kuhusu jinsi walivyofundisha – kuwatia moyo na kujadiliana namna ya kuboresha.
7. Hatimaye waanze kufundisha darasa lao peke yao. Kama kuna watoto wengi katika darasa lako, uwagawe. Walimu wapya wanaweza kuchukua darasa moja jipya. Kila darasa liwe na watoto wa umri ulio sawa. Kama kuna watoto wachache katika darasa lako, walimu wapya wafike mahali pengine kuwafundisha watoto au mnaweza kusaidiana – yaani, kwa wiki kadhaa ufundishe, kisha wafundishe kwa wiki kadhaa, na kama mwalimu mmoja hatakuwapo, mwalimu mwingine anaweza kufundisha badala yake.

Baada ya mwaka mmoja, walimu hao wapya watakuwa tayari kuwafundisha walimu wengine! Kanisa likiwa na walimu wengi, mnaweza kufanya shughuli nyingi pamoja na watoto, na kufikisha Habari Njema kwa watoto ambao hawaendi kanisani!

**Fundisha walimu kutoka makanisa mengine**

Ili watoto wote wa maeneo yote wafaidike, mtafute nafasi za kuwafundisha walimu wengine kutoka makanisa mengine. Mnaweza kubadilishana mawazo na kuwapa mafundisho uliyopokea. Kuna njia nyingi za kufanya hivyo, kwa mfano:

- Kutana na walimu wengine unaowafahamu kutoka katika makanisa mengine ili kuwaelezea ulichojifunza. Mnaweza kusaidiana kuandaa masomo, kubadilishana mawazo, kuwaonyesha mbinu mpya za kufundisha, shughuli mpya n.k.
- Zungumza na mchungaji wako ili kuandaa warsha kwa ajili ya walimu wa dhehebu lako au madhehebu yote ya eneo husika. Kama huwezi kufundisha kwa siku mbili, labda unaweza

kuendesha warsha kadhaa zilizo fupi zaidi. Utumie kila warsha kufundisha mambo machache. Uchague muda unaowafaa.

Mwisho walimu waliofundishwa, wanaweza kuwafundisha wengine katika makanisa yao na makanisa mengine pia. Kwa njia hiyo mafundisho hayo yatafika kila upande wa eneo lako na watoto wengi watafaidika.